Yale Maandiko Kwenye Ukuta

Hii ikiwa Jumatano usiku, niliahidi jioni iliyopita, pia ningenena, ikiwa Bwana angeruhusu, usiki huu, juu ya somo la; *"Yale Maandiko Kwenye Ukuta."* Ni jambo la . . . la, tungenena juu ya somo hilo kwa majuma kadha, na liwe tu nimegusa juu juu. Lakini nitajaribu kueleza tu juu juu kidogo tu kulihusu usiku huu, kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Na sasa nataka kusoma toka kwa Danieli, sura ya 5 na kifungu cha 25. Na inasomeka hivi.

Na maandiko yaliyoandikwa ni haya, MENE, MENE, TEKELI, NA PERESI.

Na sasa Bwana na aongeze baraka zake kwa huo usomaji.

2 Nami nashangaa ikiwa ndugu wetu mwema, yule mlinzi hapa, angezima hizi taa zenye mwangaza mwingi. Nina ki—ki . . . Zinaangaza kuelekea hu—huku. Asante, kwa ukarimu wako. Siwezi kuwaona wasikizi. Ninaponena na mtu ye yote, nataka kuwaangalia nyusoni ninaponena. Inaonekana kama tu ni kuwasiliana binafsi zaidi na watu.

3 Sasa twamtumainia Bwana wetu, usiku huu, tunapojaribu kupata wasaa wangu na ninene juu ya somo hili. Najua ni somo kuu. Na ni somo la ibada ya kinjilisti, na si ya uponyaji wa Kiungu. Lakini ni ya uponyaji wa Kiungu ulio mkuu sana. Mwili ulio mgonjwa sana niujuao usiku huu, ni ule mwili wa kiroho—wa Bwana wetu Yesu, duniani hapa: na umeraruliwa, na umevunjwa, hadi unahitaji sana uponyaji wa Kiungu.

4 Sasa, somo letu usiku huu linaanzia Babeli. Na Babeli kwanza ilikuwa mahali, ambapo ingaliko, huko Shinari. Na kwanza iliitwa, "lango la Mungu," *Babeli*. Babeli, na baadaye iliitwa *Babiloni,* ambayo maana yake ni "mchafuko." Na Babiloni yaonekana mwanzoni mwa Biblia, katika Mwanzo; na yaonekana katikati ya Biblia; na yaonekana mwishoni mwa Biblia, kile kitabu cha mwisho, Ufunuo. Na kwa kuwa imo kote katika Biblia, lazima ingaliko leo.

5 Na, pia, kila kitu kilichoko duniani leo, katika hali ya mambo ya kiroho, kama Roho wa Mungu na roho wa Shetani, na kila kundi la kidini na kila kitu tulicho nacho leo duniani, vilianzia katika Mwanzo. *Mwanzo* maana yake "kuanza." Na mambo hayo yote, huenda yakawa chini ya jina lingine na chini ya hali nyingine, lakini roho yule yule aliyeanzia Mwanzo, huidhihirisha. Na ni kama mti unapokua, na kukua hadi kwenye kilele chake, ambapo yote yatafikia upeo wao mwishoni, kwa

ajili ya hukumu kuu za Mungu, ambapo yeye atakapoamua mambo yote. Na yale yote yaliyokuwa na mwanzo yatakuwa na mwisho. Ni yale tu yasiyokuwa na mwanzo hayana mwisho.

6 Hiyo ndiyo sababu M—Mkristo aliyezaliwa mara ya pili hana mwisho kwa sababu yeye yuna Uzima wa Milele. Na Uzima wa Milele ni sehemu ya Uzima wa Mungu Mwenyewe, maana Mungu yu wa Milele. Na neno lile lile, neno la kiyunani Zoe ambalo lasema "Uziama wa Mungu," Yesu aliponena na kusema, "Nawapa wao Uzima wa Milele," neno hilo hilo linatumiwa tena. Kwa hivyo, mtu akizaliwa mara ya pili, roho yake imebadilishwa, naye huwa sehemu ya Mungu, hata yeye yu mwana wa Mungu. Na yeye yu wa Milele kama vile Mungu alivyo wa Milele, kwa sababu yeye yu sehemu ya Mungu, kwa Kuzaliwa kwake, Kuzaliwa kiroho.

7 Sasa, Babeli ilianzishwa na mtu aliyeitwa Nimrodi, aliyekuwa mwana wa Hamu, mtu mwovu sana.

8 Na Babeli wakati mmoja ulikuwa makao makuu ya ulimwengu. Huu mji mkuu ulipojengwa hapo, miji hii yote midogo, iliyouzunguka, ilitoa ushuru, na kodi na mengineyo, kwa mji huu mkuu, Babeli.

9 Na ndani humo, ikiwa utasoma vitabu vya kale, kama kiitwacho *Babeli Mbili* cha Hislop, na historia nyingi za kale, utaona kuwa wao walikuwa na kila aina ya mafundisho mageni humo. Walikuwa na mwanamke fulani humo, siwezi kukumbuka jina lake wakati huu, yeye angepata mizizi maalum na, toka ardhini, na kufanyia miungu kutoka kwayo. Inaaminika kuwa hiyo ilikuwa miungu ile Yakobo aliyoitwaa toka kwa baba mkwe wake, baadhi ya hiyo miungu ya mizizi na kadhalika. Ni mafundisho madogo tu, na toka kwa vitu hivyo kukazuka makundi ya . . . kidini tuyaonayo duniani leo. Ikiwa utatambua hali yake, na hali ya mambo haya leo, sawa.

10 Kwa hivyo, Babeli ulikuwa tu katika hilo bonde kuu lenye rotuba huko, na ulizungukwa na kunyunyiziwa maji na Mto Frati, na Hidekeli. Na ulikuwa kituo kikuu cha ukulima. Na Babeli ulikuwa mji mkuu. Na ni, kadiri, ya maili mia na ishirini kuuzunguka mji ule; maili thelathini kila upande, hilo lingeufanya maili mia na ishirini kuuzunguka. Wao husema barabara za mji wa Babeli zilikuwa zina upana wa futi mia mbili. Kuta zake zilikuwa na upana wa futi themanini, na urefu wa futi mia mbili kwenda juu. Wao wangefanyia mashindano ya magari juu ya hizi kuta, pamoja na magari. Na malango yalitengenezwa kwa shaba, na hayo malango basi yangekuwa na upana wa futi mia mbili. Na katikati ya mji kulikuwa na jumba la kifalme, na lile jumba lilikuwa kile kiti cha enzi. Na katikati ya ule mji ulipitia mto mkuu, Frati. Ukiuchunguza, ni mji wa ibilisi, maana umejengwa kufuatisha ule Mji wa Mungu, kama Mto wa Maji ya

Uzima mbele ya kile Kiti cha Enzi. Na katika mji huu, walikuwa na bustani kuu zilizoning'inia kutani.

11 Na lilikuwa taifa kuu, lenye nguvu kuu sana wakati huo, hadi lilikuwa limeushinda ulimwengu wote, na ulimwengu wote ulikuwa ukitoa ushuru. Ulikuwa umeendelea sana katika sayansi, na ulikuwa na vitu vya kisasa ambavyo sayansi ingeweza kutengeneza. Ulikuwa na magari mapya, mitindo mipya, silaha zenye nguvu sana, na vyuma bora sana. Ulikuwa uliojulikana sana ulimwenguni mwote.

12 Na ndipo ndani ya kuta hizi, ambamo mfalme Belteshaza alikuwa mfalme katika wakati wa tukio hili tunalonena habari zake usiku huu. Mfalme Belteshaza, ambaye Biblia yasema, "Nebukadreza, ambaye alikuwa baba yake," lakini hakika yeye alichukua mahali pa babu yake, Mfalme Nebkadreza.

13 Na wengi wenu mnakumbuka kuwa Nebukadreza alikuwa mwanzo wa ufalme wa Mataifa, kile kichwa cha dhahabu. Na alikuwa amekwenda Yerusalemu, umbali wa maili nyingi, nyingi sana, na kuwachukua Wayahudi mateka na kuwaleta chini huko katika ufalme wake, na kuwafanya watumwa, nao walitumia wanasayansi wao na kadhalika.

14 Kama tu vile Urusi ilivyofanya ilipoingia Ujerumani. Na huko ndiko walikopata bomu ya atomiki, na kadhalika, wao waliwachukua hao wanasayansi Wajerumani. Hiyo ndiyo sababu wao wameendelea sana siku hizi, waliwachukua mateka na kurudi nao huko. Wenyewe, hawakuwa na hayo, lakini walikwenda na kuvipata vitu hivyo kama tu Nebukadreza alivyowafanyia Wayahudi.

15 Nasi twatambua kwamba, katika wakati huu, kulikuwako mtu mwenye haki aliyeitwa Danieli, nabii wa Bwana, alichukuliwa mateka wakati huo. Yeye alikuwa ametumika kama mkuu juu ya wanajimu, na kadhalika, na wale wenye elimu na mamajusi, katika utawala wa Mfalme Nebukadreza.

16 Na sasa Belteshaza alikuwa ameyachukua mamlaka. Belteshaza alikuwa mtu mwovu. Yeye hakujali.

17 Na ndipo watu wote wa Babeli, walikuwa na usalama kama huo waliojisikia wanao! Mara tu walipokuwa ndani ya haya malango, na malango yamefungwa, kukiwa na kuta za futi mia mbili, upana wa futi themanini, hebu waza tu jinsi walivyojisikia salama ndani ya kuta hizo!

18 Lakini kumbuka tu hili. Haijalishi vipi sayansi imekufanya salama, Mungu atakupata utendapo dhambi! Kuna usalama mmoja tu pekee, na huo ni katika Kristo Yesu.

19 Naam, wao walivyojivuna sana kwa kuwa taifa linaloongoza ulimwenguni, mfano kamili wa ustaarabu wa kisasa, kama tu huu tunaoishi, hii Amerika ya ajabu. Nami naudhika, mimi mwenyewe, lakini nasikitika tunachukua msimamo ule ule wao

waliouchukua. Tunajivuna eti kwa maana tunao, tunavyofikiria, wanasayansi bora, na bom-bom bora sana, na bomu za atomiki, na eropleni ziendazo kasi sana na tuna aina . . . Tukiwa taifa linaloongoza ulimwenguni, tumejisikia kwa njia fulani tuna usalama pasipo Mungu.

20 Ni mfano mzuri sana. Na Mungu habadiliki kamwe. Msimamo wake kuhusu dhambi ni ule ule leo kama ulivyokuwa wakati huo. Na hakuna mahali pa kujificha hapa. Ni katika Kristo tu u salama.

21 Na katika huu mji mkuu, wao walivyojisikia hakuna njia, duniani, kwa jeshi kuvamia mji huo. Zile kuta kuu, ndefu kwenda juu, na vifaa vyao vya kisasa, na walitengwa na ulimwengu wa nje. Hawakujua kamwe kuwa taifa ovu lililoitwa Waamedi na Waajemi, ambao sasa ni Wa-Hindu wa India, hawakujua kamwe kuwa huko maili nyingi mbali walikuwa wanachimba chini ya mto, waugeuze mto Frati, kusudi wapitie chini ya kuta. Wakati wao walijisikia wako salama! Kila wakati walijisikia hivyo. Nao walipojisikia hivyo, wakaendelea kuyumbayumba dhambini.

22 Yaonekana kwamba mtu afikiapo mahali ambapo ajisikia anajitosheleza, dhambi inaanza kumchukua. Kanisa, taifa mtu binafsi, anayejisikia kuwa hataki msaada wo wote toka nje, dhambi huanza kutawala ndani yake. Hiyo ni kweli. Nasi tungetambua pia, watu waanzapo kule kujisikia kuwa wakuu sana, kila mara dhambi huingia na kuwala.

23 Kwa hivyo wao walipofunga hayo malango, walidhani wako salama. Lakini Mungu hutazama toka mbinguni! "Na dhambi ni fedheha kwa taifa lo lote."

24 Nashangaa, usiku huu, tukiwa na zana zetu zote kuu na sabmarini zinazoongozwa na atomiki, na jeti zirukazo maili mia kadha kwa sekunde, hata kuwa . . . au kwa dakika, ambazo ziendazo kasi kuliko sauti iendavyo. Lakini, usisahau kamwe, kuwa dhambi zako zitakugundua.

25 Na katika wakati huu, wao walikuwa wamefunga hayo malango. Nao walidhani wangekuwa, wangeishi kwa karamu za ulevi na ulafi kama walivyotaka kuishi, kwa maana walilindwa. Walikuwa taifa linaloongoza, mataifa yale mengine yote walilitegemea kwa sayansi na kwa—kwa msaada.

26 Na kwa hivyo, kwa wakati kama huo, kulikuwa na . . . Huyu mfalme alifikiri angejistarehesha sana. Naye alipanga tarehe ambayo yeye angekuwa na dansi kubwa mno, au kama vile ningesema, rumba ya kisasa; si mengine. Na kwa hivyo alipanga wakati, na alialika kila mtu mashuhuri, wanajeshi wote na makapteni, na wake wote na masuria.

27 Sasa, suria ni kahaba halali tu. Nanyi mwaona, mtu akijisikia ajitosheleza, hapo yeye huanza kuyumbayumba dhambini?

28 Naye aliagiza vileo vizuri sana ambavyo angalipata kwa ajili ya hii karamu ya rumba ambayo angekuwa nayo. Alidhani yu salama. Alidhani hakuna kitu kiwezacho kumdhuru, kwa sababu alikuwa salama. Naye alikuwa na pilika pilika hizi katika moja ya bustani zake nyuma ya jumba la kifalme. Na hali wakiwa nje bustanini kule, labda walikuwa wameipamba kimaridadi mno, maua yote yakimetameta, kawaleta wasichana wa maonyesho na wanawake wengi kuja kuwatumbuiza wanajeshi. Na vileo vyao na mvinyo yao! Ikiwa huo sio mtindo wa kisasa wa karamu za rumba siku hizi, sijui nyingine. Ndivyo hasa. Nao walitayarisha kila kitu, wangejumuika kweli kweli.

29 Na bila shaka wanawake wengi walioolewa walihudhuria. Waume zao waliachwa nyumbani kama yaya, hali wao walienda kujumuika. Na kadhalika, bila shaka mama alitembea sakafuni, akiwa na mtoto mgonjwa, hali mume mlevi alikwenda kujiburudisha. Ni sita tu wa kundi moja, na nusu dazani kundi lingine.

30 Nami naweza kuwaona wao walipoanza kunywa na kuburudika. Nami ningewaza jinsi bendi ingepigwa vilivyo, na kulikuwa na muziki. Na vijana walichezeshana kweli kweli. Na wanajeshi, walilewa, wakiwashika kwa tamaa wanawake na kuwapeperusha juu ya vichwa vyao, na kuwabusu na kuketi vitini mwao, na shangwe. Wakidhani walikuwa salama!

31 Ee, Amerika, yule Mungu aliyetazama na kuona hiyo karamu ya ulevi wa rumba anakutazama usiku huu!

32 Na ni furaha kuu vipi waliyokuwa nayo! Nami naweza kuwaza mfalme huyu hapa, Belteshaza, alikuwa Elvis Presley wa kisasa, yeye angefanya makuu waliyokuwa nayo. Na kufanya kwao mambo yasiyofaa, bila kujua, wakati huo wote, kuwa kifo kilikuwa mlangoni!

33 Basi, wakati karamu ilipotia fora, kama tu tamasha kuu za Hollywood ya kisasa za televisheni, wao walidhani wangeendelea kufanya mizaha mizuri juu ya dini; tuseme kama vazi la Arthur Godrey, au kitu kama hicho cha kisasa au namna ya Ernie Ford mdonoa dengu, kufanya mzaha juu ya mhubiri. Lakini Mungu yungali anatazama chini toka Mbinguni! Lakini wao walidhani waliishi katika taifa ambalo halingeweza kuguswa. Lakini unavuna unachopanda!

34 Tahadharini, enyi watu. Ikiwa u taifa, au kanisa, ua mtu binafsi, unavuna unachopanda!

35 Na, naam, naweza kumwona mfalme huyu anasimama, na kusema, "Hebuni kidogo, wasichana, hebu tufanye mzaha mzuri wakidini kuhusu mhubiri," na kadhalika.

36 Na hayo maua yote yanayometameta yakipeperuka, na wasichana wakisema, "Hewaa! Naam, nadhani tungependa kuusikia."

37 Na wale wanajeshi vijana wakiendelea kama vijana mamboleo, kwa maana hii si zaidi ya Babeli ya kisasa! Mimi ni Mwamerika, bali ndivyo Danieli alivyokuwa wa Babiloni wakati huo. Lakini hilo si udhuru ya dhambi!

Kamwambia msichana mmoja siku moja, "Je, wewe u Mkristo?"

Akasema, "Nakufahamisha, ni Mwamerika."

Nilisema, "Hilo halifai cho chote." Hata kidogo!?

38 Nafurahi kuwa Mwamerika, lakini hilo halihusiani kwa vyo vyote vile na Ukristo; hata kidogo. Tukitenda dhambi, tutahukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu, na uhakikishiwe hilo.

39 Wao walikuwa na nabii huko, lakini hawangemsikiza. Walikuwa na Ujumbe, lakini walitaka kuufanyia mzaha.

40 Ikiwa hiyo si Amerika ya kisasa. Siijui. Wao wana Injili, ile kweli, lakini huidhihaki.

41 Basi, walisema, "Na twende huko tukavichukue hivyo vifaa vya watakatifu wanaojigaragaza, na tuvilete hapa tukavifanyie mzaha."

42 Mungu hawaruhusu wenye dhambi kuwadhihaki watu Wake! Mtalipia hiyo, siku moja.

43 Nao walienda wakachukua vyombo vya Bwana, na wakavileta hekaluni, na watakuwa na kinywaji kizuri wakitumia vyombo hivyo vya Bwana. Nao walitia mvinyo uitwao Oertel's 92 au Pabst Blue Ribbon, ndani, wavitumie kwa mzaha, lo, waligonganisha hizo bilauri pamoja na hivyo vyombo, na wakaanza kunywa, na kucheka na kuifanyia mzaha dini ya Bwana. Hawakujua walichokuwa wakitenda.

44 Na ndivyo lilivyo taifa hili, usiku huu, hawajui wamekataa Ujumbe wa Bwana Yesu Kristo, katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuzaliwa mara ya pili.

45 Ingawa wao walikuwa wa kidini, sasa, hiyo karamu ya rumba ya walevi, wao walikuwa wa kidini, kwa maana Biblia ilisema kuwa, "waliisifu miungu yao."

46 Hivyo basi waweza kuwa wa kidini sana, na hali umekosea! Naam. Sio unyofu. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti." Kwa hivyo wao walikuwa na kanisa kuu la taifa, na dini ambayo wangeitumikia, nao walivifanyia mzaha vitu vitakatifu vya Mungu.

47 Na hilo ni mfano halisi wa siku hizi, kufanyia mzaha vitu vitakatifu vya Mungu. Wao huwaita watu, wanaojaribu kuishi maisha mema na maadilifu, na manyofu, huwaita "wa mtindo wa kale" au "watakatifu wanaojigaragaza," au majina fulani ya kashfa. Nao huita vipawa vya Bwana, ambavyo Yeye anavitenda, "kutenda kwa pepo mchafu, kama mpiga ramli au ibilisi." Ee, mwawezaje kuepa hukumu? Ile damu

ya wafia imani inalia dhidi yake. Mungu asipolihukumu taifa hili kwa ajili ya dhambi yake ya kisasa, itambidi Yeye aiinue Sodoma na Gomora, na aombe msamaha kwao kwa kuwaangamiza. Hiyo ni kweli. Tunaelekea kuhukumiwa! Na maajabu haya makuu mnayoyaona Mwokozi wetu aliyebarikiwa akitenda, ni ishara za kuonya, kuwa hukumu imekaribia; nayo yamesambazwa kote katika taifa hili toka upande hadi upande, toka Mashariki hadi Magharibi, toka Kaskazini hadi Kusini. Nao wameyakataa, wameyachekelea, wameyalaumu wameyaandika katika magazeti yao kama "Upuzi." Waza hilo, Babeli ya kisasa!

48 Sasa walipokuwa wakinywa, wakigonganisha vikombe vyao wakinywa; kwa ghafula, wakati huyo mchezaji mashuhuri mpenda anasa, aliyeitwa Belteshaza, alipokuwa tu tayari kunywa kutoka kwa kikombe chake, macho yake yakabenuka alipogeuka na kutazama kuelekea ngomeni, maana yeye aliona, ukitoka mbinguni, mkono wa Mwanadamu, na ulianza kuandika juu chini ukutani.

49 Nawatakeni mtambue, Uliandika kwenye plasta. Sasa, labda ile mishumaa ilikuwa karibu na mapambo yao, ambapo wao walikuwa wanacheza rumba yao ya kisasa, na taa zilikuwa zikiangazia ukutani. Mungu hatendi mambo pembeni! Ni papo hapo mwangani, ambapo Mungu hunena na kutenda. Kwa hivyo maandishi Yake ya kimbinguni yalikuwa kwenye plasta ya ukuta machoni pao wote.

50 Na hapana budi mfalme aliyaona kwanza, huyu mpenda mizaha wa kisasa, mchekeshaji mzuri redioni, mchezaji wa televisheni. Alipoinua bilauri anywe, ama kikombe, alichokuwa nacho mkononi mwake, macho yake yakabenuka, naye akatetemeka sana. Nafikiri alitetemeka. Biblia ilisema kuwa, "Mifupa yake ikalegea." Bila shaka alitetemeka sana, hakika. Mungu aanzapo kuonyesha ishara Zake, ni wakati wa kutetemeka. Naam. Na kama yeye alivyotambua, wimbo wake wa rumba ulimfanya atetemeke.

51 Na ndipo yeye alipoyaona haya maandishi ukutani, naweza kuwaza huyo msichana amejipaka midomo yake rangi sijui kama nini, na nywele zake zote zimepambwa, na akicheza akizunguka-zunguka pamoja na hawa wanajeshi walevi, alisema, "Nashangaa imekuwaje kwa mvulana huyu usiku huu?" akikekevua.

52 Na mvulana mmoja akamshika, na kusema, "vema, na tucheze hii inayofuata pamoja nawe." Na muziki ukakoma.

53 Oh, hili taifa kuu lenye dhambi, wakati mmoja rumba zenu zitakoma! Ikiwa hamtasikiza sauti ya mhubiri, mtausikia mkono wa Mungu katika hukumu siku moja. Lakini rumba zitakoma, kama tu vile zile bendi zilivyofanya, zilizocheza, *"Karibu na*

wewe, Mungu wangu," katika Titanic. Siku moja mtabadili wimbo huo.

54 Na muziki ukakoma. Na wao walimwona yule mfanya mizaha wao hodari, mchezaji mashuhuri wa televisheni, na, yeye alikuwa amesimama, magoti yake yakigongana, alipotazama na kuona hili jambo kuu likitendeka. "Mbona," yeye alisema, "tumezungushiwa kuta. Walinzi wangu wamesimama mlangoni, walio bora sana."

55 Lakini, mwaona, Mungu si lazima apitie malangoni, jinsi mdhanivyo. Yeye alishuka toka utukufuni! Na mkono Wake ulikuwa ukiandika ukutani.

56 Na upesi, wakiwa mahali pa kisasa, Biblia ilisema yeye aliwaita wachawi wake wote, mamajusi, na maaskofu wote, madaktari na mapapa, na makadinali, na kadhalika. Na kusema, "Sasa niwaambieni, wangwana, nimewapa ruhusa kuhubiri na kutenda mliyotaka kutenda. Sasa nitafsirieni, mimi yaliyo ukutani."

57 Lakini kama ilivyokuwa tu wakati huo, ndivyo ilivyo sasa, hawakuwa wamezoea ya kimbinguni. Hawakujua lo lote kuyahusu. Hawakujua kutafsiri lugha zisizojulikana. Hawakujua lo lote kuhusu lugha ya Kimbinguni. Nao walishikwa na bumbuwazi. Hawakujua lo lote kuihusu. Na wote waliposimama hapo . . .

58 Kumbuka, huku ni kule kuanzishwa kwa ufalme wa Mataifa. Na kama ulivyoanza kwa ya kimbinguni, utakwisha kwa ya kimbinguni.

59 Lakini hawa maaskofu na makadinali, na madaktari wakuu, hawangeweza kutafsiri ya kimbinguni. Hawakujua lo lote kuyahusu. Walitazama kote vitabuni vyao vya sanaa, na hawakupata cho chote ambacho kingelinganishwa na hicho. Mwaona, vitu vya kiroho hueleweka kiroho. Na ndipo wao wote wakasumbuka, nao hawakujua la kutenda.

60 Na, mwishowe, malkia mdogo. Kumbuka, yeye hakuwako kwenye karamu hiyo ya rumba. Na njia pekee ambayo yeye alijua kitu fulani kilikua kikitendeka, neno lilimjia kuwa mfalme amehangaika, na karamu imekomeshwa. Yeye angalikuwa mmoja wa waumini wazuri. Na, kwa njia moja au nyingine, yeye alikuwa mmoja ambaye hakusahau.

61 Malkia akaingia upesi karamuni mle. Na alipomwona yule mfanya mizaha wa kisasa amehangaika, na bendi yake yote, akasema, "Ee, mfalme, uishi milele!" Lakini yeye hakujua alikuwa mfu papo hapo. Kasema, "Uishi milele! Najua kuwa ninyi nyote mmehangaishwa na maandiko yale ukutani. Nami naona hawa papa, na maaskofu na makadinali, na wale wenye shahada za theologia, na hakuna ye yote wao awezaye kuyasoma. Bali, ee, mfalme, hebu na nikwambie jambo fulani! Yuko mtu katika ufalme wako, anayejua ya kimbinguni."

62 Ee, ndugu, tunapoona maandiko kwenye ukuta, leo, lakini kunaye mtu ajuaye kuyahusu. Huenda umepitia katika afisi za kila daktari mjini, na wao walikwambia, “Sharti utakufa.” Lakini kunaye Mtu! Huenda umeyumbayumba dhambini hadi nafsi yako ni nyeusi kama kuta zenye masizi za kuzimu, nawe u tayari kujinyonga, pasipo tumaini. Lakini kuna Mtu, na Jina Lake ni Yesu! Yeye ajua ya kimbinguni. Naye yu ufalmeni mwetu, maana sisi tu wana wa Ufalme Wake. Kunaye Mtu!

63 Kasema, “Ajua ya kimbinguni, maana miaka mingi iliyopita Roho wa Mungu alionekana akikaa ndani yake. Naye ana Roho njema kupita kiasi. Yeye angetafsiri ndoto, aliona maono, na kila moja yao ilikuwa tu sahihi. Basi, msisumbuke, nipeni dakika chache nami nitamleta hapa.”

64 Siku moja utamwendea! Huenda usiwe na nafasi yake nyumbani mwako. Una shughuli nyingi, ukitazama televisheni, ukicheza karata, ukinywa pombe, ukihudhuria karamu za dansi. Lakini kuna wakati mmoja utakaomwendea. Naam.

65 Na kwa hivyo Danieli akaletwa. Na alipoletwa . . . Mhubiri wa haki, mtu wa Mungu! Singeweza kuwaza mtu wa Mungu aishi mahali kama hapo ila awe alikuwa ameipinga. Lakini, mwaona, yule mfalme hakuitilia maanani, hiyo ndiyo sababu yeye alikuwa katika hali aliyokuwamo.

66 Na wao walimleta Danieli, naye akasema, “Mbona mapapa na madaktari wenu wasiwatafsirie?” Wao hawakuwa na cho chote cha kutafsiria.

67 Hivyo basi nini ilitendeka? Danieli alisema, “Ee, Belteshaza, ulijua mambo hayo yote. Hayakufichwa kwako.”

68 Nami naiambia Amerika! Natumai ningewafanya, kwa dakika hii, wasikie sauti yangu. Mwafahamu mambo haya yote! Kama mataifa yaliyotangulia yalivyotenda dhambi na kutenda yale tumetenda, tumepimwa katika mizani, nasi tumeonekana kuwa tumepungukiwa. Kipi kilitendeka kwa Ufaransa? Kipi kilitendeka kwa Ujerumani? Kipi kilitendeka kwa mataifa mengine walioelekea kwa “mvinyo, wanawake, na kujiburudisha”? Kila mara huwa hivyo, nasi si wasioweza kupatwa na hukumu. Mungu yu mwenye haki.

69 Naye alisema, “Baba yako, jinsi Mungu alivyomfanya taifa kuu, lakini yeye alisahau. Naye alitenda mambo yale yale unayotenda, na Mungu akamgeuza awe mnyama wa porini.” Kasema, “Ijapokuwa ulijua hayo yote, umevichukua vyombo Vyake vitakatifu na kuvifanyia mzaha.” Tazama, Yeye alisema, “Hayo maandiko yamewekwa kwenye ukuta, na wakati huu ufalme wako umehesabiwa.” Yaani, “Tazama hapa, ewe, siku zako zimehesabiwa! Ufalme wako umeondolewa kwako na kupewa taifa lingine, taifa katili, lisilomcha Mungu,” ambalo—ambalo ni baya kama wao walivyo. Mungu hufanya dhambi ipigane na dhambi. Nastaajabu, leo!

70 Kwa wakati uo huo, hebu niseme kwanza, yeye alipokuwa amesimama pale, akitazama Maandiko hayo kwenye ukuta, hakujua kamwe kuwa hapo chini ya malango, wakati uo huo, wale walinzi walikuwa wameuawa. Na wale wanajeshi walikuwa katika njia za mji, wakiwaua walinzi wa jumba la mfalme. Walikuwa kwenye vipandio. Na hao wanawake wakisimama hapo, mbali na watoto wao wachanga, mbali na waume wao, na waume mbali na wake zao, wote wamelewa, wakisikiza aina fulani ya dansi ya kisasa na kufanya yasiyofaa. Na wanajeshi walikuwa kwenye vipandio na katika dakika chache mfalme angeangamizwa. Na kundi hilo la wanaume walevi lingeangamizwa, na taifa lisiloamini kuwa kuna Mungu, lililopagawa na shetani. Na hao wanawake wangevuliwa mavazi yao, wasichana na kadhalika, na kunajisiwa barabarani; kisha wangewatwaa kwa visigino na kupasua vichwa vyao kutani. Wakawakatakata baada ya kuwanajisi; wanajeshi wazimu, walevi! Ilikuwa mlangoni, maana wao walipimwa katika mizani, nao wakaonekana kuwa wamepungukiwa.

71 Nami nashangaa, siku hizi, katika maovu yetu yote ya kisasa, kucheka kote na kufanyia mizaha ibada za uponyaji, kuchekelea na kufanyia mizaha kanisa la Mungu aishiye, na kuendelea kama Biblia ilivyosema wao wangefanya, "wakatili, wenye kujivuna, wenye mfano wa utaua, bali wanakana nguvu zake."

72 Nashangaa, siku hizi tunapodhani tu salama sana, na, kwa ghafula, twaona kuwa Urusi i miaka mitano mbele yetu, katika sayansi.

73 Tumekuwa katika karamu nyingi sana. Tumeyumbayumba sana dhambini. Kanisa limelala sana, halijali mikutano ya maombi tena. Hawajali. Wao hunena dhidi ya Roho halisi na wa kweli wa Mungu aishiye; Hawamtaki. Wao ni wa kidhehebu sana, wamejipamba sana! Hawana wakati wa kuhudhuria mikutano ya maombi, wao wako kwenye televisheni na sinema, na kutangatanga hapa na pale, na kwenye karamu za ulevi na kadhalika. Hiyo ni kweli!

74 Hilo laweza kuonekana kama la mtindo wa kikale, lakini ndilo taifa linalohitaji siku hizi. Kuna kutenda kike kwingi sana kwa Injili, pamoja na mipira ya kuvalia mikononi. Sharti lishikwe kwa mikono mitupu, kwa Roho Mtakatifu. Kweli!

75 Billy Graham alisema, yapata juma moja au mawili yaliyopita katika moja ya jumbe zake, alisema, "Taifa hili laweza kuwa Kibaraka wa Urusi, wakati wo wote Urusi itakapo." Tuko wapi?

76 Mtanunua rekodi za Elvis Presley, na mkae nyumbani mkatae kwenda kanisani ili msikize *Twampenda Susana,* hivi karibuni! Mmepimwa kwenye mizani, mmeonekana kuwa mmepunguka! Imekuwaje! Kuna maandiko ukutani!

77 Warusi walirusha Sputniki ambayo hatuwezi kufanya cho chote juu yake, maili mia tano toka duniani; na wangeweza kuweka nusu dazani juu ya Amerika katika dakika thelathini zijazo. Na kutoa mwito na kusema, “Jisalimisheni au mtakuwa majivu kwa dakika chache.” Wao waweza kulitenda. Hakuna cho chote tuwezacho kufanya kuwazuia. Liko mikononi mwao, wakomunisti wamwaga damu, wasio na huruma, wasiomcha Mungu. Hayo ndiyo Mungu anayotumia kufanya dhambi iwe dhahiri. Hakika ndivyo. Ukisoma Biblia, Urusi haina budi kutenda hivyo kulingana na Ufunuo. Vema, ninyi waalimu wa unabii mwaweza kutofautiana na Hilo, lakini ngoja hata itakapotimia. Urusi imewekwa hapa kwa kusudi hilo. Biblia ilisema hivyo.

78 Sasa hapa ina Sputniki. Tulijaribu kurusha moja majuzi usiku, tukidhani tungefanya kama wao walivyofanya; ikaruka futi tatu toka ardhini, ikakoma. Dansi na dhambi nyingi kupindukia! Tumepimwa katika mizani, nasi tumeonekana kuwa tumepungukiwa. Mungu, uturehemu!

79 Tutafanyaje? Ingekuwaje kama wangetuma hizo Sputniki pamoja na makombora hayo, na kusema, “Jisalimisheni, la sivyo, mtakuwa chungu la mavumbi katika dakika tano?” Bila shaka, serikali yetu, kuokoa maisha, ingejisalimisha. Hilo tu ndilo jambo pekee wawezalo kufanya.

80 Basi ingekuwaje kwa baadhi yenu Waamerika, sisi sote ndani hapa; si hapa tu, lakini nanena kuhusu taifa lote? Nikinena kitaifa.

81 Enyi vipusa mamboleo, wasichana mnaokwenda huku na huko hali midomo yenu imepakwa rangi kama chipukizi la ua la waridi; na mgemchekelea mhubiri pembeni, akihubiri Injili. Nawe tineja, unayefikiria eti una akili zaidi ya vile ulivyo na busara ya kuitumia!

82 Itakuwaje kwenu, baba mnaoketi nyumbani usiku na mama na kutazama televisheni hali kijana wenu yuko vichochoroni, na binti yuko huko kwenye viburudisho, mahali fulani, naye yuko huko akizisakata rumba zake? Nanyi mnatazama televisheni, na kuidhihaki Injili!

83 Itakuwaje kwenu, enyi washiriki wa kanisa? Matokeo yenu yatakuwa nini? Huenda jina lako likawa katika kila kitabu, au kanisa kubwa zaidi mjini; bali usipokuwa chini ya usalama wa Damu ya Bwana Yesu, utaangamia pamoja na hao watakaoangamia, hakuna tumaini kwako.

84 Itakuwaje? Sputniki imo kule juu. Na kipi kingetendeka? Taifa lingejisalimisha bila shaka, hilo tu ndilo jambo bora serikali iwezalo kutenda.

85 Ndipo ingekuwaje? Wimbi baada ya wimbi, la meli zilizojaa wanajeshi; wimbi baada ya wimbi, la aeropleni, zingetua katika

taifa hili. Wanawake wangenajisiwa barabarani. Mngefanyaje? Ni yao. Mtafukuzwa nyumbani mwenu, watalitwaa.

86 Itakuwaje kwenu vijana wa kike na kwenu vijana wa kiume, na ninyi nyote wakati huo? Dhambi lazima ilipiwe. Haijalishi ni taifa gani, wala ni nani, anayeifanya. Kibinafsi, au kitaifa, italipiwa! Na kundi la wanajeshi wakomunisti walio wakatili, wasiomcha Mungu, waliojaa sharafa mashavuni, wangewakamata wake zenu na kuwanajisi, hata binti zenu. Na mngesimama na mlipende, hamuwezi kufanya lo lote.

87 Nini chanzo chake? Kwa sababu mmesikiza upuzi wa vitu kama vipindi vya televisheni vya rumba na dhambi, na wahubiri baridi wa kidesturi tu wasioweza kutafsiri ya kimbinguni. Maandiko yako kwenye ukuta! Naam! Nasi tumepimwa kwenye mizani, na kuonekana kuwa tumepungukiwa.

88 Hayo yangetendeka lini? Kabla mapambazuko asubuhi. Ni nani atakayeyazuia? Jaribu. Biblia ilisema yatatendeka.

89 Lakini hebu niwaambieni, hayo hayatagusa kanisa la Mungu aishiye, tutakuwa tumeandoka wakati huo!

90 Kwa hivyo, rafiki, sikiza. Ikiwa kitu hicho ki karibu sana, nasi twayaona maandiko kwenye ukuta, hakuna cho chote kiwezacho kukomesha jambo hili lisitendeke sasa.

91 Amerika imekwisha kuhubiriwa, ya kimbinguni yametendwa, nao wanaendelea huyumbayumba moja kwa moja juu yake.

92 Kwenda nchini mahali fulani na ufanye mkutano wa ufufuo na uwe na waongofu arobaini katika juma; na urudi huko baada ya majuma sita, huna wanne. Kile kidimbwi cha kale kimevulia hakina samaki tena. Mungu anao kiasi fulani ambao amewachagua. Na yule wa mwisho aingiapo, hilo lafunga ule mlango na imekwisha.

93 Ndipo hakuna cho chote kilichobaki ila hukumu rehema zinapokataliwa. Na hapa tuko mwishoni mwa njia. Ya kimbinguni yanatendwa, yanachekelewa na kufanyiwa mzaha. Na jambo la mwisho, Mungu ameshakuja katika nguvu Zake Mwenyewe, katika Mwanawe Mpendwa, kutenda kupitia kwa Kanisa Lake, nao husema ni "Kuabudu roho za wafu," au "Shetani". Imebaki nini tena ila hukumu? Na hapa kuna maandiko kwenye ukuta.

94 Lakini ikiwa hiyo imekaribia hivyo, na kila mwalimu ajua kuwa kanisa lanyakuliwa kabla ile dhiki haijaanza. Kwa hivyo ikiwa hiyo imekaribia hivyo, ingetendeka kabla asubuhi, na kunyakuliwa, je? Kumekaribia kuliko hivyo! Ee, Jina la Bwana libarikiwe! Kuja kwa Bwana kumekaribia. Maandiko yameandikwa, na yameandikwa ndani ya Biblia, nasi tutayaona maishani mwetu.

95 Nanyi, je, kwa ushawishi wa sauti yangu, mtapokea Yesu Kristo wakati huu? "Tubuni mkabatizwe," Petro alisema "kila mmoja wenu, katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na watu wote walio mbali. Maana hapana jina jingine chini ya mbingu waliopewa wanadamu litupasalo kuokolewa kwalo." Isipokuwa uwe wa Kristo! Huenda ikawa u Mmethodisti, Mbaptisti, Mpentekoste, Mnazarini, Mkatoliki, umepotea isipokuwa uwe wa Kristo! Na Kristo anapoingia ndani yako, ni kuzaliwa upya na Roho Mtakatifu. Mpokee usiku huu, tunapoomba.

96 Vichwa vyetu vikiwa vimeinama. Nashangaa tu juu ya hili, wangapi hapa wanaojua kuwa jambo hili kuu lingetendeka? Huenda ukaenda kulala usiku huu pamoja na mkeo, na asubuhi yake amekwenda. Ninyi, baba na mama, mwaweza kubusu watoto wenu wakalala, usiku, na kesho asubuhi kile kitanda kidogo kiwe kitupu. Nanyi mtakimbia barabarani, kuona kipi kilichompata Bibi Yones, yeye pia amekwenda. Kule kunyakuliwa kumekaribia, Biblia inaonyesha dhahiri.

97 Na katika mkutano huu, wakati ungali na nafasi, kama tu mwanamume mwe—mwenye busara, na mwanamke mwenve busara, mbona usiutii mwito huo ulio moyoni mwako, na kusema, "Bwana Mungu nijaze na huo Uzima wa Milele." Kwa maana ikiwa roho yako ingali ina nia ya kielimu, wewe u wa dunia hii. Lakini Roho wa Mungu, aliyetoka Mbinguni, huja moyoni mwako na kukupa Roho Mtakatifu, ndani yako. Ile dhiki ijapo, yule Roho [Roho Mtakatifu] atarudi kwa Muumba Wake, nawe utaenda pamoja Naye. Haijalishi u wa kidini vipi, hutakwenda ila tu kuwe na Kitu fulani humo cha kukupeleka.

98 Ni wangapi usiku huu, hali vichwa vyenu vi—nainamishwa, mbele ya Ujumbe huu, mngemwinulia Kristo mikono yenu, na kusema. "Mungu, nijaze Roho Wako Mtakatifu. Na wewe ukija, nataka kwenda pamoja nawe?" Mwaweza kuinua mikono yenu? Mungu awabariki, kote kanisani. Bila shaka, mikono mia mbili au zaidi iko hewani.

99 Rafiki mwenye dhambi, ikiwa hujampokea Kristo kamwe, waweza kwa wakati huu kuinua mkono wako, na kusema, "Bwana Yesu, unirehemu mimi?" Mungu akubariki wewe, bibi. Mungu akubariki wewe hapa, nyuma huko. Mtu mwingine, "Nikumbuke tu, Bwana." Mungu akubariki wewe uliye hapa, chini hapa. Bwana awe nanyi. "Nikumbuke, Ee, Bwana. Macho yangu yamefunguliwa hivi sasa. Natambua kuwa labda nimekiri kuwa Mkristo kwa muda mrefu, lakini sijawahi kujua maana ya kuzaliwa mara ya pili. Sijampokea Roho Mtakatifu kamwe."

100 Kwa hivyo, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuingia katika Ufalme, wala hawezi hata kuuona huo Ufalme."

101 Waweza kuinua mkono wako, na kusema, "Nirehemu mimi, Ee Roho Mtakatifu. Na ujapo kuchukua Kanisa, nichukue mimi?" Mungu akubariki wewe, bibi. Na mwingine, "Nikumbuke, ee, Mungu." Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bibi. "Nikumbuke mimi, Ee Mungu." Akubariki wewe hapa, kijana. Mungu akubariki wewe huko. Nyuma huko, msichana, nyuma huko. Nawe uliye kule nyuma bibi. "Unirehemu, ee Mungu, niyaonapo yale maandiko kwenye ukuta. Nina busara kutosha, tusema, kuona kuwa yale yamesemwa kutoka katika Biblia, usiku huu, kuwa haya ni marudio ya historia."

102 Tuko mwishoni. Hakuna cho chote kiwezacho kusaidia. Kile kitu kitakachouangamiza ulimwengu kimo mikononi mwa watu wenye dhambi.

103 Kunao tu wachache zaidi. Huenda wewe ukawa yule wa mwisho aliyechaguliwa kuja kwa Kristo. Huyo wa mwisho ajapo, hukumu itaingia; kitu kimoja kimepunguka, hicho chaweza kuwa ni wewe. Je, utampokea yeye usiku huu hali tukingoja?

104 Mikono mingine ishirini, thelathini imeinuliwa. Sasa hatuna mahali hapa pa kutoa wito wa madhabahuni, kuwaleta watu hapa mbele, kwa sababu hatuna mahali po pote. Lakini nitawaulizeni ninyi, hakika, oh, iweni waaminifu na muisikize sauti ya onyo. Iweni waaminifu na mkaombe Kristo dua, papo hapo mnapoketi, "Bwana unirehemu mimi, mwenye dhambi, na unipokee kabla sijapita ng'ambo ya pazia ya rehema. Kabla sijatenda dhambi nikamaliza siku yangu ya neema, unirehemu, Bwana," na Yeye atafanya hivyo. Sasa ombeni hivyo ninapoomba pamoja nanyi.

105 Bwana uliyebarikiwa, tumesimama katika hali ya kuogofya usiku huu. Tunaposoma Neno Lako, na kujua kuwa wakati wo wote redio ingetoa onyo kwa ghafula, na bendi za rumba zianze kuimba, *"Karibu na wewe, Mungu Wangu,"* lakini itakuwa imechelewa sana wakati huo, hukumu imeingia. Makombora yameelekezwa kwetu. Uharibifu, kwa maili baada ya maili, na tani baada ya tani ya—ya nguvu za atomiki zinazoifagia dunia, na kadhalika, ambazo zingeteketeza ulimwengu mzima. Na ziko mikononi mwa watu wenye dhambi. Na Biblia ilisema kuwa hivyo ndivyo itakavyotendeka. Nasi twaona yale maandiko kwenye ukuta.

106 Ee Bwana Mungu, mimi sistahili kujaribu kuleta Ujumbe kama huu kwa watu. Nami najisikia jinsi nilivyo mdogo, nikisimama hapa, kujaribu kueleza somo kama hilo, lakini unisamehe kwa sehemu yangu ya kutoweza kufanya hivyo. Lakini kwa njia moja au nyingine, toka moyoni mwangu, nakuuliza wewe uuingize Ujumbe huu, jinsi utakavyo mioyoni mwao, maana naona ile saa ikija. Na uturehemu Mungu, na umwokoe kila mmoja, na uwajaze na Roho Mtakatifu. Na wao

wawe watoto wako, waliofunikwa Kiungu katika wema wako, na wapate usalama kwa Bwana Yesu.

107 Maana, taifa letu haliko salama. Tumedhani tuko salama. Ndivyo hata na ule Ufalme wa Babeli ulivyodhani, lakini, wakati huo wote, taifa ovu lililokuwa likifanya kazi. Na kulikuwa na taifa ovu likitenda kazi, hata sasa twajua kuwa wametushinda, nasi tuko chini yao.

108 Bwana, Kanisa liko chini ya rehema zako. Wao wataangamiza; lakini wewe utalitwaa Kanisa Lako. Ee, Bwana, tutwae tuwe chini ya ulinzi Wako, usiku huu. Na utubariki kwa ajili ya Yesu; na katika Jina Lake twaomba. Amina.

109 Kwa upole sana, kwa dakika moja hivi. Iweni wanyenyekevu.

> Kwa upole na upen do Yesu aita,
> Akuita wewe na . . .

Tunapoimba sasa, jihoji.

> Langoni Yeye anangoja na kutazama,
> Kukutazama wewe na mimi.
>
> Njoo Nyumbani, (Wapi? Panda huku, panda huku juu.)
> Enyi mliolemewa, njooni Nyumbani;
> Kwa mkazo na kwa upole, Yesu aita,
> Aita, Ee mwenye dhambi, njoo Nyumbani!

[Ndugu Branham aanza kuvumisha wimbo *Kwa Upole na Upendo*—Mh.]

110 Jamani, je, si utakuwa wakati wa ajabu kwa hilo kutendeka sasa! Jamani, ni vema, wakati wo wote yeye yu tayari. Amina! Nafurahi sana kumjua Yeye. Nafurahi sana kuwa huu mwili mzee unaokunjamana, unaodhoofika hapa, utageuzwa kwa dakika moja, kufumba na kufumbua macho. Nitakuwa kijana tena, niishi milele.

> Wazee watakuwa vijana milele,
> Watageuzwa dakika moja;
> Wasiokufa, tutasimama katika mfano wake,
> Watang'aa zaidi ya nyota na jua.

Ni nafasi ya jinsi gani! Usimkatae.

> Ee, vipi utakavyomtaka Yeye aseme, "Umefanya vema,"
> Katika siku hiyo ya milele!
> Usimkatae Mwokozi mpendwa moyoni mwako,
> Usimkatae. (Na huu uwe ndio usiku huo.)

111 Ni wangapi wanaompenda Yeye kwa mioyo yenu yote, nanyi mko tayari Yeye akija? Lo, shukrani jinsi gani! Je, hujisikii kama uliyesuguliwa sasa, ndani? Ile Injili, tunasafishwa kwa maji ya

Neno. Geuka upande mwingine, ukamsalimie mtu fulani kwa mkono, useme, "Mungu akubariki. Najisikie vizuri sana. Mungu akubariki, ewe msafiri. Mungu akubariki, dada, ndugu." Tu wasafiri njiani.

> Nikitembea kwenye barabara kuu ya kale,
> Nikitangaza po pote niendapo,
> Bwana, heri niwe mkristo wa mtindo wa kale,
> Kuliko cho chote nijuacho.

112 Sasa hali tuko katika wakati huu wa uchaji wa Mungu, naamini tumechelewa sana kufanya mstari wa maombi. Na . . . Naamini Roho Mtakatifu amefurahia sana, huu umati mkimjia Kristo. Sasa jitafutie kanisa upesi sana, ubatizwe na uende kanisani humo, kanisa nzuri lililojazwa na Roho, na ukabaki humo maishani mwako mwote.

113 Ni kazi zipi Kristo alizoahidi atazitenda? Yeye alisema "Kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya." Basi, Uwepo Wake uko hapa. Naam, najua, marafiki. Ni—najua, bila shaka, kuwa Yesu yuko hapa. Kuna Mtu hapa, ni mtu yule yule aliyetembea Galilaya. Ni Mtu yule yule aliyekukomboa wewe kwa Damu Yake, na kukuponya wewe kwa kupigwa kwake. Na Yeye yuko hapa kufanya na kutenda kila kitu alicho fanya, kwa sababu ni Bwana Yesu yule yule.

114 Sasa na tuombe kwa muda mchache, pole pole. Na mwe tu katika maombi hali nikijaribu kupata nia ya Roho Mtakatifu [Ndugu Branham anyamaa kidogo—Mh.]

115 Kwa hivyo, huo muziki mtamu, jinsi watu walio matesoni usiku huu wangependa kuusikia! Watu ambao labda waliketi kwenye viti mnavyokalia usiku huu, wameisikia Injili na kuaga dunia, walio matesoni usiku wa leo, jinsi hao wangependa kuketi kwenye hivyo viti mnavyokalia; imechelewa sana sasa. [Ndugu Branham ananyamaa kidogo—Mh.]

116 Bwana, wewe uliyeziumba Mbingu na nchi, wewe uliyemtuma mbarikiwa Bwana Yesu hapa duniani; na katika Yeye ulikaa utimilifu wa yule Roho. Nawe umekwisha kusema, kupitia kwa kinywa Chake, "Mimi ndimi mzabibu, nanyi ni matawi. Mzabibu wenyewe hauzai matunda, bali matawi huzaa matunda." Naomba, Mungu, kuwa wewe utajidhihirisha Mwenyewe usiku huu, kati yetu, ili watu hawa wapate kujua kuwa Ujumbe ambao umekwishahubiriwa, watoka Kwako, ya kwamba unatuonya tujitayarishe, na zile siku za mwisho zimekaribia.

117 Huenda kukawa na watu walio wagonjwa wanaoketi hapa Bwana. Wape moyo, wapate kuponywa, maana twaomba hili kwa utukufu wa Mungu. Sasa, Bwana, tunajinyenyekeza wenyewe kwako, kama kanisa la Mungu aishiye; kuona, nafikiri, kila mkono ndani hapa uliinuliwa. Nami nitakuuliza Wewe, usiku huu, Bwana, kutufanyia kitu fulani maalum. Na tujalie

hivi sasa ya kwamba watu hawa waweze kujitolea sana hivi kwamba Roho Mtakatifu angepitia kwao, kwa imani kama hiyo, na ili kwamba nipate kujitolea Kwako, Nawe ukapate kutenda kazi kupitia karama Zako na kujithibitisha Mwenyewe miongoni mwetu; maana, huenda kukawa na wageni miongoni mwetu. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

118 [Nafasi tupu kwenye kanda—Mh.] . . . maana Yeye kila mara huonyesha yesha rehema kabla ya hukumu. Nitawauliza wahudumu wabaki huko, na waombe. Na tuombe.

119 Na sasa, hasa, nimekuwa nikuhubiri, nami—nitawauliza labda ninyi watu mlioko mbele hapa, au po pote mlipo, hebu anzeni kusema hili. Biblia yasema kuwa, "Yeye yu kuhani mkuu awezaye kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu." Vema basi, ikiwa Yeye ni Kuhani Mkuu aliyekuwa jana, ni Yeye yule leo; ndipo kutenda Kwake kule kule alikotenda jana, Yeye atatenda leo ikiwa Yeye ni yule yule. Sivyo? Kwa hivyo ikiwa Yeye aweza kuguswa sasa, mguse kwa mambo yako ya udhaifu, na Yeye akujibu.

120 Waza tu, Yeye aliposimama karibu na umati kama huu siku moja, mtu alikuja, aliyeitwa Petro, au jina lake lilikuwa Simoni. Na Yeye alisema, "Jina lako ni Simoni. Wewe u mwana wa Yona. Lakini tangu leo, utaitwa Petro." Yeye alikuwa nani? Yule mtume aliyependwa.

121 Filipo alipokutana na Nathanieli, na akaja huko, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli kweli kweli ambaye ndani yake hamna hila," yaani, "Mkristo, mtu mwaminifu."

Kasema, "Je, ulinijuaje, Rabi?"

122 Kasema, "Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya ule mti, nilikuona."

123 Yule mwanamke aliyekuwa na ugonjwa wa kutoka damu alijitokeza. Yeye akatazama makutano wale.

124 Wao walidhani kazi Zake zilikuwa za shetani, nao wakasema mioyoni mwao, "Yeye ni Beelzebuli." Naye akatambua mawazo yao. Sivyo?

125 Yeye alisema, "Sitendi lo lote isipokuwa Baba anionyeshe kwanza. Na kazi nizifanyazo, nanyi pia mtazifanya." Kwa hivyo yeye sharti kuwa hivyo, ikiwa anafanya kazi katika kanisa Lake, kwa sababu hilo ni Neno Lake.

126 Sasa nataka kuwaulizeni. Ikiwa makutano haya, watu wawili au watatu, Bwana atawajalia imani kutosha kugusa vazi Lake, na Yeye atarudi katika Roho Wake, na kutenda yale hasa aliyotenda alipokuwa hapa duniani, je, mngeridhika kumkubali kama mponya wenu? Je, mngekubali? Semeni, "Amina, ikiwa mngekubali. [Makutano wasema, "Amina"—Mh.] Na aliruhusu, ndilo ombi langu. Sasa ninyi ombeni tu. Na ikiwa ninyi . . .

127 Ni watu wangapi walio wagonjwa ndani humu wanaotaka kuponywa, inueni mikono yenu. Kila mahali tu, vema, watu walio wagonjwa wanaotaka kuponywa.

128 Sasa ikiwa kunaye yote katika jengo hili, ambaye mimi . . . simjui ye yote ninayemtazama.

129 Nafikiri huyu ni Rosella anayeketi hapa, msichana aliyekuwa na wa ulevi, aliyeitwa na Bwana mkutanoni mahali fulani, alikuwa mlevi kupindukia na madaktari walikuwa wamemkatia tamaa. Yeye, alipoitwa na Bwana, huyu msichana ajua sikuwa nimemwona wala kumjua. Na Bwana alimwambia yote kuhusu maisha yake na hali yake, na akamwambia kuwa angepata nafuu. Na ndiye huyu hapa usiku huu, tuzo la neema ya Mungu. Mwenye ugonjwa wa ulevi hata daktari baada ya daktari alimkatia tamaa, hata kile chama cha kuwasaidia walevi. Namjua.

130 Lakini kwa vingine, nina hakika kuwa huyu ndugu anayenitazama, anayeketi hapa na suti ya kijivujivu, yeye ndiye ndugu anayetuletea maua. Naamini hivyo ni kweli. Si—siwezi kukumbuka jina lake sasa. Kitambo kidogo kilichopita yeye alikuwa nyumbani kwangu, pamoja na ndugu Boze; Shultz, Ndugu Shultz.

131 Mbali na hao, nafikiri nilimwona Ndugu Fred Sothmann muda mfupi uliopita, mahali fulani jengoni humu, lakini nimesahau sasa mahali alipokuwa. Ingawaje, yeye alikuwako, yuko hapa mahali fulani.

132 Nasi—simjui ye yote mwingine. Lakini Mungu awajua ninyi nyote. Ikiwa mtaweza tu kuomba na kumwuliza Mungu, ijaribuni imani yenu.

133 Na mtu ye yote asisogee po pote sasa. Iweni watulivu sana kwa muda mchache ujao. Sasa, *"Amini tu,"* mkiweza. Na kwa unyenyekevu sana mwenzavyo kwa muda mchache, na mketi mkiwa kimya. [Mpiga kinanda apiga, *Amini tu.*—Mh]

134 Waza tu, Kristo aliliahidi. "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mtaniona Mimi, maana Mimi . . . Mimi, si mwingine." *Mimi* ni neno la kumtaja mtu. "Mimi nitakuwa pamoja nanyi hata ukamilifu wa dahari. Mambo nifanyayo mimi, nanyi pia mtayafanya." "Yesu Kristo Yeye yule jana, leo na hata milele." Ni kweli? Sharti iwe kweli.

135 Vema namshukuru sana Bwana. Ninge . . . mwaweza kuviinua vichwa vyenu mkitaka.

136 Papa hapa pembeni, kuna mwanamke anayeketi papa hapa pembeni. Ni mwanamke mweusi. Bibi sikujui. Mungu akujua. Lakini kuna ile Nuru juu ya mwanamke huyu sasa. Yeye ana . . . Ikiwa Bwana atanifunulia shida yako ni nini, na kile unachoombea, je utaamini kuwa ni Bwana

Yesu atakayekusaidia? Ni lazima una shida, au kitu fulani unachotaka, maana iko hapo.

137 Mnaona, marafiki, ninyi mnasema. “Vema, siioni.” Hiyo yawezekana kuwa hungeiona. Naitazama moja kwa moja. Mwaona? Mwasema, “Vema, Ndugu Branham, ikiwa waweza kuiona kwa hisi zako, naweza pia.” Ah, sivyo.

138 Paulo aliiona Hiyo, yule Yesu katika mfano wa Nuru, na wale waliokuwa pamoja naye hawakuiona. Waona? Wale mamajusi waliiona ile Nyota, ile Nuru iliyowaongoza, lakini hakuna mwingine ye yote aliyeiona. Ni kwa watu fulani tu. Ni vipawa.

139 Mwanamke huyu ana shida ya mapindi. Hiyo ni kweli. Pia una ugonjwa wa moyo. Ndivyo hasa. [Yule mwanamke asema, “Utukufu! Haleluya! Asante Yesu! Haleluya!”—Mh.] Sikiza. Jina lako ni, wanakuita Essie. [“Naam.”] A-a. Jina lako la mwisho ni Upshire. [“Naam, Ndugu Branham.”] Unaishi kwenye barabara iitwayo Cleveland Kaskazini. Anwani yako 1264. Ndivyo hasa. [“Hapo ndipo ninapoishi.”] Wako. . . Uligusa kitu fulani, bibi. Wewe unajua hukunigusa mimi kamwe.

140 Huyo msichana anayeketi kando yako hapo, yeye pia anaomba. Naye anamwombea mtu mwingine, na mtu huyo ni, mama yako, ana shida katika mapafu yake. Nawe una uhusiano fulani na mwanamke huyu *hapa*, wewe u binti-mkwe wake. Na jina lako ni Margaret. Hiyo ni kweli. Nanyi huishi mahali pamoja. Nawaona mkija, na kuingia.

141 Unawazaje kuihusu, bwana, ewe mtu wa pili unayeketi hapo? Je waamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu? Je, waamini? Ikiwa Bwana atanifunulia shida yako ni nini, je, utamkubali? Una ugonjwa wa tumbo. Naam. Ikiwa ndivyo, simama. Ndivyo hasa. Wewe ni mhubiri.

Bila shaka, mnasema, “Yeye anayatazama mavazi yake ya wahubiri.”

142 Vema, mbali na hilo, mtu fulani anadhani wewe ni mpresbiteria, lakini wewe ni mhubiri Mpentekosti. Hiyo ni kweli. Amina. Wasiwasi wako umekufanya uwe na vidonda tumboni. Vimepona. Nenda nyumbani ukapate afya, ndugu. Amina. Iweni na imani katika Mungu! Msiwe na shaka!

143 Wawazaje, unayeketi papa hapa? Naam. Je, waamini? Unaamini kuwa mimi ni mtumishi wa Mungu? Au wataka kitu toka kwa Mungu? Ikiwa Mungu atanifunulia kile utakacho, je, utaamini kuwa la kimbinguni linatendeka? Waamini ni yale yale ambayo Yesu angesema? Kwa moyo wako wote? Una kivimbe, na kivimbe hicho kiko kwenye nyonga yako. Hiyo ni kweli. Nawe pia una ugonjwa wa tumbo, unatokana na hali ya wasiwasi. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Eva May. Readman ndilo jina lako la mwisho. Unaishi kwenve barabara ya mji, 1378 Magharibi barabara ya 13. Hayo ni kweli. Ili ujue kuwa mimi ni mtumishi wa Mungu, huyo ni binti yako mdogo anayeketi pale. Unataka

maombi kwa ajili yake. Msichana huyo anatokwa na damu, nayo humtoka anaposhitushwa sana au anapolia sana. Hayo ni BWANA ASEMA HIVI. Huyo mvulana mdogo ni ndugu yako. Naam. Huyo mvulana mdogo, naye, unamtakia maombi. Yeye anasumbuliwa na kufunga choo, naye pia amepoteza uzito mwingi hivi majuzi. Sivyo? Hilo ni BWANA ASEMA HIVI.

144 Yule mwanamke mweupe anayeketi kando yako, yaonekana kama kwamba anasumbuliwa na jambo fulani. Je, waamnini dada? Waamini Mungu amemtuma Mwanawe, Yesu Kristo, kukitangazia kizazi hiki cha Mataifa kuwa Yeye yuaja upesi? [Dada asema, "Naam, bwana."—Mh.] Una shida ya tezi inayokuumiza, na pia una ugonjwa wa chango, nawe una wasiwasi. Hutoki kwenye mji huu, hata hivvo. Unatoka Detroit. Nambari yako, unakoishi, ni 12134 barabara ya Fandler. Hiyo ni kweli. Detroit, Michigan. Wewe ni Mtaliano. Jina lako ni Viola P-o-l-o-f. . . Polofmba. E-eh. Uwe na imani katika Mungu, upate kupokea unachohitaji.

145 Wawazaje wewe, chini upande *huu*? Je, waamini kwa moyo wako wote?

146 Nawe je, msichana unayeketi hapo? Je, waamini kwa moyo wako wote, msichana uliye mwisho hapo? Vema, mmoja wenu, haijalishi. Wadhanije, wewe hapo unayemfuatia? Je, unaamini kwa moyo wako wote maskini mama unayeketi, ukinitazama mimi? Je, wawazae kuhusu hili? Waamini kuwa Bwana Yesu angeponya mishipa iliyovimba ya damu uliyo nayo? Waamini? Labda ungewaza hili, ungeamini zaidi ikiwa ningekuambia mume wako alikuwa na shida ya masikio. Ulitaka aombewe. Hivyo ndivyo hasa. Sasa unaniamini? Hukuwa ukiipata hapo mbeleni. Hilo lilikuamsha, kwa sababu ulipokea kuponywa kwako wakati huo.

147 Uliinua mkono wako, kando yake, bibi. Wawazaje juu ya haya? Waamini kuwa Mungu angekuponya? [Yule mwanamke asema, "Najua Yeye ataniponya."—Mh.] Utafanya hivyo? Vema, basi yabisi kavu yako itakuondokea.

148 Nawe bwana waonaje? Wewe uliyepunga mikono yako. Unaamini Mungu angekuponya ugonjwa wako wa moyo, na kukupa afya? Je, waamini Yeye atakuponya?

149 Wewe unayeketi, ukimtazama yeye hapo, je, waamini pia? Wataka Mungu. . . ulikuwa na ugonjwa wa moyo pia, sivyo? Naam. Nawe ulikuwa na ugonjwa wa sukari, pia. Ndiyo. Je, waamini Mungu atakuponya? Basi waweza kuupokea.

Je, waamini? Mwaminini Mungu!

150 Vipi chini ndani *hapa*? Wewe, bwana, unayeketi hapa mwishoni mwa viti, unaamini? Inakupasa kuwa nayo, umeponywa tu sasa hivi. Unaona? Ulikuwa na ugonjwa wa mguu, sivyo? Waamini kuwa Bwana Yesu. . . Lakini unamwombea mtu mwingine sasa, huyo ni ndugu yako. Naye yuko Wisconsin.

Amepasuliwa mapafu hivi majuzi nusu yakaondolewa. Naam. Unaamini? Basi waweza kupokea kile unachoomba. Ee, Jina la Bwana libarikiwe!

Nitamsifu, Nitamsifu.
Nitamsifu Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa
ajili ya wenye dhambi;
Mpeni sifa enyi watu,
Kwani Damu Yake imeosha kila waa.

151 Bwana mbarikiwa, tutakuona wewe siku moja ukija toka juu mbinguni. Twajua wewe uko hapa sasa katika Mwili wa kiroho, umejidhihirisha mwenyewe kikamilifu kwetu. Ulimwengu hauwezi kuyasoma hayo, Bwana. Hata hatuutarajii uyasome, kwa sababu wewe ulisema. "Hawataniona tena." Lakini tunajua kuwa Una watoto wawezao kukuona wewe. Tuna watoto wakujuao wewe. Nasi tunakushukuru kwa ajili yao.

152 Nasi twaomba sasa ya kwamba utavuma kote jengoni humu, pamoja na Roho Mtakatifu aliye mkuu, na uponye kila mtu aliye mgonjwa ndani humu. Hivi sasa jipatie utukufu, Bwana. Na watu wasiketi katika ufu, bali wao waamke na kuangaza, na—na kumpa Mungu sifa na utukufu. Katika Jina la Yesu.

153 Ikiwa mnamwamini, simameni na kumpa Yeye sifa kwa mioyo yenu yote. Na furahini katika Bwana Yesu, maana Yeye sasa aponya kila mmoja wenu, kwa ajili ya utukufu Wake mkuu wa kiungu. Bwana awabariki. Amina.

Yale Maandiko Kwenye Ukuta SWA58-0108
(The Handwriting On The Wall)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatano jioni, Januari 8, 1958, katika Shule ya Sekondari ya Lane Tech kule Chicago, Illinois, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org